

EVERGREEN PROFESSIONAL RECOVERIES, INC 12100 NE 195TH ST #125  
BOTHELL, WA 98011  
1-800-241-1305

TAREHE

Mlipaji:

Nambari ya Akaunti Yetu:  
Nambari ya Kumbukumbu:  
Maelezo ya Kosa:  
Tarehe ya Kosa:  
Namba Pleti ya Gari:  
Kiasi cha Kulipa: \$

**NOTISI**

Unajulishwa kwamba Jiji la Albuquerque limeruhusu huduma zetu zikusanye deni unalodaiwa la Faini ya Mfumo wa Kutoza Faini Kiotomatiki kwa Kuendesha Gari kwa Kasi. Jiji la Albuquerque limeweka Programu ya Kutoza Faini Kiotomatiki kwa Kuendesha Gari kwa Kasi ili kupunguza ajali ya magari na vifo vya wapita njia na waendeshaji baiskeli vinavyohusiana na kuendesha magari kwa kasi. Ikiwa unapokea Notisi hii, akaunti inayorejelewa hapo juu imechelewa kulipa faini inayodaiwa na unahitaji kuchukua hatua ya kulipa faini hiyo mara moja.

Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa ya faini hii au kuomba kupewa adhabu ya kutoa huduma kwa jamii badala ya kulipa imepita. Tafadhali lipa kulingana na maagizo yaliyo hapa chini haraka iwezekanavyo. Ikiwa una maswali kuhusu faini yako, tafadhali wasiliana na ofisi yetu kwa nambari 1-800-241-1305 chaguo la 2 kuanzia saa mbili asubuhi (8:00 am) hadi saa kumi na mbili jioni (6:00 pm) saa za Mountain Standard Jumatatu hadi Ijumaa.

Matokeo ya kukosa kulipa na kuwa na zaidi ya deni moja la faini ya mfumo wa Kutoza Faini Kiotomatiki kwa Kuendesha Gari kwa Kasi (ASE, Automated Speed Enforcement)

Ikiwa mmiliki aliyesajiliwa ana madeni mawili (2) au zaidi ya faini za mfumo wa ASE, mmiliki aliyesajiliwa anaweza kuchukuliwa hatua zinazoweza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na lakini si tu kuzuiwa kugesha gari katika vituo vya maegesho, kuzuiwa kuendesha gari na/au kukamatwa kwa gari lake ikiwa gari lake litapatikana limeegeshwa kwenye barabara yoyote au kando ya barabara ndani ya Jiji la Albuquerque; kwenye au katika kituo chochote cha maegesho kinachomilikiwa na Jiji; kwenye au katika kituo chochote cha maegesho kinachosimamiwa na Jiji; au kwenye jengo lolote linalomilikiwa na Jiji ndani ya viziwi vya Jiji la Albuquerque. (8-5-1-43 ROA 1994).

**TAFADHALI LIPA UKITUMIA MOJAWAPO YA NJIA ZIFUATAZO:**

\* Lipa kwa Barua:

Cheki au Hawala ya Fedha (Money Order) (HAKUNA KULIPA PESA TASLIMU) [Usilipe kwa kampuni ya Evergreen Professional Recoveries.] Lipa kwa: Kitengo cha Kutoza Faini Kiotomatiki

PO Box 593095

Orlando, FL 32859-3095

Tafadhali hakikisha unajumuisha nambari ya kumbukumbu iliyo hapo juu kwenye cheki au hawala yako ya fedha (money order).

\* Lipa kwa Simu au Wasiliana nasi ili uweke mpango wa kulipa:

Tafadhali wasiliana na Kitengo cha Kutoza Faini Kiotomatiki (Automated Enforcement Division) bila kutozwa kwa nambari (866)247-8157 ili ulipe wakati wowote, usiku na mchana, kila siku. Saa za Huduma kwa Wateja ni Jumatatu hadi Ijumaa saa mbili asubuhi (8:00 am) hadi saa tisa alasiri (3:00 pm) (MT).

Nambari ya Siri: 2554

\* Lipa au Angalia Mtandaoni:

Unaweza kuangalia picha na video za kosa lako mtandaoni na ulipe faini yako kupitia: [www.ZeroFatality.com](http://www.ZeroFatality.com). Namba Pleti: 28923UNM

Nenosiri: RxThT9PM

\* Lipa mwenyewe:

NI: Pesa taslimu, Cheki ya Kulipwa kwa Keshia au Hawala ya Fedha (Money Order) ndizo tu njia za kulipa mwenyewe zitakazokubaliwa.

{HAKUNA CHEKI ZA BINAFSI, HAKUNA MALIPO KUPITIA KADI ZA MIKOPO AU ZA BENKI} Lipa kwa Automated Enforcement Division One Civic Plaza, Chumba cha Chini cha B2090, Albuquerque, NM 87102 Jumatatu hadi Ijumaa: Saa mbili asubuhi (8:00 am) hadi saa kumi na moja jioni (5:00 pm) (MT)